



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**  
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/02/80**

**31 Oktoba, 2024**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi ya **Afisa Habari Daraja la II ZPSE-10 (Nafasi 1 – Unguja)** kwa ajili ya **OFISI YA RAIS - KATIBA SHERIA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:-**

**Sifa za Muombaji:**

1. Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
2. Awe na Vyeti halisi vya kumalizia Masomo.
3. Awe Mwenye Shahada ya kwanza ya Uandishi wa Habari (Journalism) au mawasiliano ya umma (mass communication) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Majukumu:**

1. Kutayarisha na kupitia vipeperushi na matangazo ya kuitangaza Taasisi.
2. Kuweka kumbukumbu za matukio muhimu ya Taasisi.
3. Kupiga picha za mnato na picha za video na Kutunza picha, Maktaba na marejeo.
4. Kutayarisha vipindi, Makala na vielelezo vyengine,
5. Kuandaa majarida na mabango (Posters).
6. Kukusanya takwimu zinazohusu habari.

7. Kufuatilia taarifa za Taasisi katika vyombo vya habari vikiwemo mitandao ya kijamii, redio, televisheni na magazeti na kuwasilisha kwa mamlaka husika.
8. Kupokea maoni na hoja za wananchi, kuzifuatilia na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kwa lengo la kufanyiwa kazi.
9. Kuandika ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
10. Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

### **Jinsi ya Kuomba:**

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe **31 Oktoba, 2024** hadi tarehe **08 Novemba, 2024**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini [www.zanajira.go.tz](http://www.zanajira.go.tz).
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-  
**KATIBU,  
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,  
S.L.P 1587,  
ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:  
KATIBU,  
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**